UNIVERSITY OF AMSTERDAM

UvA-DARE (Digital Academic Repository)

# Foreign direct investment and poverty alleviation in Tanzania: a case of Bulyanhulu and Geita Gold Mines Limited in Kahama and Geita districts

Nyankweli, E.M.

**Publication date**
2012

Link to publication

**Citation for published version (APA):**
Nyankweli, E. M. (2012). *Foreign direct investment and poverty alleviation in Tanzania: a case of Bulyanhulu and Geita Gold Mines Limited in Kahama and Geita districts*.

**General rights**
It is not permitted to download or to forward/distribute the text or part of it without the consent of the author(s) and/or copyright holder(s), other than for strictly personal, individual use, unless the work is under an open content license (like Creative Commons).

**Disclaimer/Complaints regulations**
If you believe that digital publication of certain material infringes any of your rights or (privacy) interests, please let the Library know, stating your reasons. In case of a legitimate complaint, the Library will make the material inaccessible and/or remove it from the website. Please Ask the Library: https://uba.uva.nl/en/contact, or a letter to: Library of the University of Amsterdam, Secretariat, Singel 425, 1012 WP Amsterdam, The Netherlands. You will be contacted as soon as possible.

*UvA-DARE is a service provided by the library of the University of Amsterdam (https://dare.uva.nl)*
Download date:14 Aug 2022

# Muhtasari

Utafiti huu unahusu uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni na kupunguza umaskini nchini Tanzania na umejikita katika uchunguzi wa sekta ya uchimbaji madini ya dhahabu (BGML na GGML). Utafiti huu umelenga kubainisha athari za uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika maisha ya jamii ya vijijini na vilevile juu ya uchumi wa kitaifa na kimkoa. kupima madhara ya kiuchumi, kijamii na kimazingira yatokanayo na uchimbaji mkubwa wa dhahabu kama sehemu ya uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni Tanzania na mchango wake katika kupunguza umaskini, hilo ndilo lengo kuu la utafiti huu. Licha ya kutupatia mwanga juu ya mafanikio ya kiuchumi, kijamii na hasara zake, lengo jingine ni kuangalia ushirikiano kati ya serikali na makampuni binafsi kwa kuchambua na kuchunguza sera ya uwajibikaji kwa jamii ya makampuni ya madini kama njia mojawapo ya kukabiliana na umaskini. Mkakati wa madini umekuwa moja ya vipengele muhimu katika sera zinazopendekezwa kwa ajili ya maendeleo, matumizi sahihi ya ukuaji na mafanikio katika sekta ya madini yanaweza kuchangia kupunguza umaskini. Hata hivyo, tafiti nyingi za hivi karibuni zinatoa taarifa matokeo hasi kuhusu Tanzania na nchi nyingine za kiafrika kushindwa kutumia vema fursa ya madini na maliasili zake kupunguza viwango vya umaskini. Utafiti huu haulengi kupingana na matokeo ya tafiti za awali, bali unanuia kutoa mwanga kuhusu mchango wa sekta ya madini katika uchumi wa Tanzania. Ukuaji wa katika sekta ya madini unachangia maendeleo ya tanzania japo kwa kiasi kidogo lakini ni muhimu sana hasa kwa jamii za vijijini ambazo ni maeneo ya moja kwa moja yanayopakana migodi. Taarifa ya utafiti huu imepangwa katika sura ya nane kama ilivyoainishwa katika aya zifuatazo.

Sura ya kwanza inahusu utangulizi inazungumzia Tanzania na sababu iliyopelekea kufanyika utafiti huu. Imefanya mapititio ya sera ya mageuzi ya kiuchumi kama inavyohusika na uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni kabla ya uhuru, baada ya uhuru na wakati wa mageuzi ya uchumi. Pia inaelezea kuhusu hali kijamii,kiuchumi, kijiografia na mwenendo wa idadi ya watu wa Tanzania ikilinganisha na ukuaji wa uchumi na sekta

ya madini. Katika sura hii maeneo ya utafiti yamebainishwa katika ukanda wa dhahabu wa ziwa Victoria, sifa za eneo hili na sababu za uteuzi wake. Sura ya pili inahusu uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni, umaskini, uwajibikaji wa kampuni za madini kwa jamii na mabadiliko ya hali ya maisha. Sura hii inachambua dhana za umaskini, uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni, na uwajibikaji wa makampuni ya madini kwa jamii kinadharia na matendo ili kuelewa mahusiano yaliopo katika kupunguza umaskini. Pia inatoa mwanga kihistoria juu ya maisha ya Wasukuma (jamii yenye watu wengi katika ukanda huu) na vitongoji vya machimbo ya dhahabu (GGML na BGML hasa) katika zama za tatu, kabla na baada ya uhuru na kipindi cha sasa. Katika sura hii pia kunajadiliwa hali ya kijamii na mwenendo wa idadi ya watu kwa sasa katika maeneo kunakopatikana madini hususani kwenye uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni. Sura ya tatu inaelezea mbinu za utafiti kwa kutoa maelezo ya uchambuzi wa mfumo wa hali ya maisha(Livelihood Analytical Framework), ubunifu wa utafiti na utekelezaji wake. Inaweka katika mtazamo dhana ya kaya katika uchambuzi, mchakato sampuli na maswali ya utafiti kama yalivyotumika katika utafiti. Pia imeainisha aina ya taarifa na namna ya ukusanyaji wa taarifa hizo, mbinu za uchambuzi na hali halisi ya zoezi la ukusanyaji wa taarifa za kitafiti.

Sura ya nne inachambua sheria na sera ya madini, mafanikio ya uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika Tanzania kwa kuangalia fursa za sheria ya sasa na vikwazo vya sheria iliyopita katika kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika sekta ya madini. Hii imefanyika kwa kutazama hali ya uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni kabla na baada ya mageuzi uchumi kisekta na uchumi kwa ujumla. Sura ya tano inaangazia athari za kijamii na kiuchumi zitokanazo na uchimbaji wa madini, kwa kuweka mbele faida ya kiuchumi na hasara za sekta hiyo. Inaelezea hali ya mapato ya ndani, mapato ya fedha za kigeni, ajira na madhara mengine ya kijamii na uzoefu katika vitongoji kunakopatikana migodi ya madini. Sura ya sita inazungumzia athari za kimazingira na kiafya zitokanazo na uchimbaji wa madini kwa kufanya uchambuzi wa shughuli mbalimbali za mazingira na majanga ya uzembe kama matokeo ya shughuli za madini. Mambo yaliainishwa hapa ni uharibifu wa ardhi, aina mbalimbali ya uchafuzi wa mazingira na madhara kwa afya ya binadamu, nchi, wanyama na mimea.

Sura ya saba inahusu uwajibikaji wa makampuni kwa jamii katika sekta ya uchimbaji madini nchini Tanzania. Sura hii inachambua sera ya uwajibikaji wa makampuni kwa jamii ili kuweka bayana umakini na tabia ya kampuni za madini katika dhana nzima au uwajibikaji kwa jamii. Inafuatilia mbinu na utekelezaji wa mipango ya uwajibikaji kwa jamii wa makampuni ya madini katika jitihada za kupunguza umaskini, kuweka taswira nzuri kijamii na uchimbaji madini endelevu wa madini. Imebainishwa kuwa makampuni ya madini yamebuni sera za mashirikiano na jamii, misingi ya kanuni za usalama, heshima, maadili na uwajibikaji. Sera hizi zinasisitiza katika kushughulikia matatizo ya jamii zikizingatia na kutambua malengo ya maendeleo ya mikoa na taifa. Uwazi, vigezo, ufuatiliaji, utoaji taarifa na uchimbaji endelevu vimeelezwa bayana katika sera za makampuni yote ya madini. Sera ya uwajibikaji kwa jamii ya makampuni ya madini inazingatia kubuni maeneo ya ubora katika utekekelezaji wa mipango ya uwajibikaji kwa jamii. Maeneo hayo ni pamoja na ubora wa afya na ustawi wa jamii, elimu, mafunzo na ujuzi wa maendeleo, maendeleo endelevu ya kiuchumi, uwezeshaji wa wanawake na maendeleo ya miundombinu vijijini. Uwajibikaji kwa jamii kwa makampuni ya madini hufanywa aidha na makampuni ya madini peke yake au kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa, serikali za mitaa, na asasi za kijamii. Makampuni yameabuni idara za maendeleo na uhusiano na jamii ndani ya miundo ya mashirika yao ambazo zina wajibu wa kusimamia na kutekeleza miradi ya uwajibikaji wa makampuni kwa jamii. Hadi sasa makampuni yameshawekeza pesa za marekani $ 35,700,000 katika miradi ya uwajibikaji kwa jamii kati ya 1999 na 2005.

Sura ya nane ni hitimisho na mapendekezo ya sera. Utafiti umegundua ya kwamba mafanikio ya miradi ya madini ni pamoja kusaidia kupambana na umaskini kwa njia ya ukuaji uchumi na maendeleo endelevu. Imeonekana pia uwekezaji katika uchimbaji wa madini wa makampuni ya kigeni umetoa ajira na ujuzi mbalimbali, utoaji wa elimu ya afya na huduma za jamii. Ni kweli tunajua kwamba uwajibikaji wa makampuni kwa jamii unahitaji kujitolea na kuzingatia kanuni za maendeleo ya jamii ili kuleta ufanisi kwa jamii ambayo inaweza kusaidia kuepuka hali mbaya ya kiuchumi, kijamii na mazingira. Uwajibikaji huu pia unajikita kikamilifu katika juhudi za kupunguza umaskini kama

zianavyoanishwa na dira ya Tanzania 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania.

Hata hivyo, si kila kitu king'aacho ni dhahabu. Ajira katika sekta ya wachimbaji wadogo wa madini imeshuka wakati mapato yanayotokana na sekta hiyo yamekuwa chini, kwa maana ya kwamba, mapato katika sekta ya wachimbaji madini wadogo yamepungua kwa kiasi cha dola za kimarekani 44 bilion ukilinganisha na dola za kimarekani 1.2 bilioni zilizovunwa na wachache waliobahatika ajira katika makampuni ya kigeni, hii ni punguzo la mara 36 zaidi. Utafiti huu umeonyesha uhusiano chanya kati ya uzalishaji wa dhahabu, katika mashirika ya kimataifa na ukuaji wa ajira kwa kiasi kikubwa. Ajira imeshuka mno kwa wataalamu wa Tanzania na kada zingine kutokana na uwekekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika sekta ya madini. Hivyo, utafiti unakubaliana na hoja kwamba maendeleo ya sekta ya madini katika Tanzania yana mchango muhimu katika uzalishaji, mapato, teknolojia na mauzo ya nje, wakati imekuwa na mchango kiasi kidogo wa kiuchumi (mchango katika Pato la Taifa) licha ya kuwa katika hatua yake ya awali. Basi imebainika kuwa, kuvutia uwekekezaji wa moja kwa moja wa kigeni nchini ni hatua kubwa peke yake tofauti na manufaa ya uwekezaji huo. Pamoja na mafanikio katika kuvutia uwekekezaji wa moja kwa moja wa kigeni, sera ya sasa nchini inahitaji marekebisho ili kuweza kusimamia vema manufaa ya mali asili na kukabiliana mapungufu yaliyomo katika ugawanaji wa mapato yatokanayo na mali asili za taifa.

Utafiti huu unadhihirisha kuwapo mabadiliko ya wazi ya maisha katika vitongoji madini ya katika bonde la dhahabu la ziwa Victoria. Hizi ni alama za maboresho katika hali ya kiuchumi na kijamii kwa wakazi wa maeneo ya kunakopatikana madini ikilinganishwa na mazingira vijijini yanayofanana na haya, ukiachilia mbali mapungufu katika masuala ya mazingira na afya. Utafiti huu pia unabainisha ya kuwa makampuni ya uchimbaji madini na serikali yameendelea kuweka hatua madhubuti ili kupunguza madhara ya shughuli za uchimbaji madini ili kuhakikisha maendeleo endelevu. Mipango ya usimamizi wa mazingira ni pamoja na namna ya kuzuia uchafuzi wa mazingira, udhibiti wa taka, ulinzi na kurejesha rasilimali za ardhi na maji na kwa ajili ya kuondoa au kupunguza athari mbaya ya mazingira. Hata hivyo, utafiti huu umeonyesha kwamba athari zaa mazingira hazipewi kipaumbele kama ilivyo haja ya mgawanyo mzuri wa mapato ya madini, si kwa

sababu si muhimu lakini kana kwamba haina mahitaji ya haraka katika mipango ya juhudi za kupunguza umaskini (kwa kuwa madhara ya kimazingira huchukuwa muda mrefu kubainika). Pia ni wazi kwamba makampuni ya madini yamewanufaisha wananchi kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa sera zake za uwajibikaji kwa jamii na kwa manufaa yasiyo ya moja kwa moja (multiplier effect) kutoka makundi mbalimbali ya wafanyabiashara na makandarasi ambao wanafanya shughuli zao katika vitongoji vya uchimbaji madini kufuatia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika sekta ya madini kwa jamii za vijijini . Licha ya michango inayotolewa kwa jamii kuwa ya hiari, wananchi na Serikali wamevutiwa na juhudi hizo.

Kwa jumla utafiti unahitimisha kwa kusema uwekekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika sekta ya madini umeleta maendeleo Tanzania pamoja na kwamba matokeo haya kuwa madogo ikilinganishwa na sekta nyingine kubwa na kwa maeneo maalum. Tuna budi kutazama mambo matatu mahimu wakati wa kuchunguza athari hizi za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kuhusu uchimbaji wa mkubwa wa madini katika Tanzania. Kwanza, ni mapato yatokanayo mauzo ya nje, ajira, na teknolojia, ujuzi na maarifa, na mapato ya Serikali ambayo ni muhimu katika masuala jamii, kufuatana na misingi dhaifu ambayo sekta ilianzia katika miaka ya 1990. Pili, ukiachilia mbali mapato yanayotokana na mashirika ya kimataifa, na athari za kijamii kwa uharibifu wa mazingira yatokanayo na shughuli za uchimbaji wa madini, thamani ya mchango wa makampuni ya madini ya kimataifa katika jamii ni dhahiri, kutokana na mahitaji makubwa ya huduma mbalimbali za kijamii, kiuchumi na miundombinu. Tatu, matokeo ya maendeleo ya uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika sekta ya madini ni yametiwa dosari zaidi kutokana na kukosa mguso wa moja kwa moja kiuchumi na sekta nyingine kama inavyoelekezwa na nadharia ya "trickle-down".

Matokeo haya matatu, kwa kutafakari historia ya Tanzania kisiasa, kiuchumi na mwenendo wa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni na umiliki binafsi wa nguzo kuu za uchumi. Kwa sasa Tanzania imeingia katika mfumo huria wa kiuchumi ambao umebomoa misingi ya sera za serikali za udhibiti uchumi zilizoasisiwa na Azimio la Arusha mwaka 1967. Katika hatua hii mpya nchi imelazimika kutoa motisha mbalimbali

kwa wawekezaji kama kupunguza viwango vya kodi au kusamehe kodi katika mitambo ama bidhaa zihusuzo uwekezaji katika sekta ya madini ili kurudisha imani ya wawekezaji wa moja kwa moja wa kigeni ambao tayari walishaathirika sana na hatua zilizichukuliwa wakati wa Azimio la Arusha. Kwa hiyo, serikali haina budi kukubali kukosa baadhi ya faida zake kutumika kama motisha ya wawekezaji ili kufidia hatari ya mtaji (risk on capital) na kuwa na matarajio kunufaika baada ya muda mrefu ya miaka 20-25. Motisha hii ilikuwa na nia ya kurejesha imani kwa wawekezaji kuwa wanaweza kufanya biashara Tanzania na kupata faida na hivyo kuwezesha hali ya kasi ya mtiririko wa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni nchini Tanzania, wakati ikirekebisha mazingira ya uwekezaji wa nje kwa faida ya nchi, lengo ambalo limetimia kwa kiwango kikubwa.

Hivyo, mapato ya chini kwa hazina ya serikali ni dhahiri, lakini ongezeko la uzalishaji na mauzo ya nje kwa upande mwingine pia teknolojia muhimu na ujuzi vinapatikana Tanzania mara baada ya miaka kumi ya kwanza ya uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni katika sekta ya madini. Hii ni ishara nzuri ya hatma ya serikali kupata mapato yake inayotarajia katika miaka kumi ijayo, ambapo uwekezaji zaidi unatazamiwa hivyo serikali ya kunufaika zaidi. Kuona mguso wa moja kwa moja wa sekta ya madini katika uchumi kiujumla itakuwa vigumu kwa sekta ikizingatiwa kuwa sekta ya madini ni sehemu ya nguzo ndogo ya uchumi ukilinganisha na nguzo zingine zilizopo kama kilimo na viwanda, japokuwa mchango wake katika mauzo ya nje huonekana zaidi. Hali hii ni kwa sababu ya bei ya juu ya madini katika siko la dunia.

Hali ya wasiwasi kijamii na kimazingira imezingatiwa pia katika uchunguzi wa uchimbaji madini ulioendelevu na sera ya madini kuhusu ya shughuli za makampuni makubwa ya madini katika Tanzania. Kuna ongezeko la maambukizi ya maambukizi ya VVU / UKIMWI katika jamii inayozunguka migodi. Katika utafiti huu imebainika kuwa shughuli za Madini ni moja ya sababu zilizochangia ukuaji wa miji midogo na soko la bidhaa, pia vijana wenye fedha na wanawake, wameongeza hatari ya kuenea kwa ugonjwa wa VVU / UKIMWI. Hata hivyo VVU/UKIMWI ni tatizo lihunaolohusu sekta zote katika jamii ya Watanzania, na kutishia kupunguza ukuaji wa uchumi na kupunguza mafanikio katika umri wa kuishi. Masuala ya Mazingira yanayotajwa katika utafiti huu ni

kama mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa mazingira, uchafuzi wa hewa, uchafuzi wa maji na uchafuzi kelele. Pamoja na kwamba, GGML na BGML hufanya tathmini ya athari za kijamii na kimazingira zihusuzo shughuli zao yaani EIAs, bado kuna mambo mengi ya kufanyika ili kuondokana au kupunguza athari mbaya jumla za kijamii na mazingira ili kupata maendeleo endelevu katika Bonde la dhahabu katika ziwa Victoria.

Sera ya madini ya Tanzania na mfumo wa kisheria uliopo umekuwa maarufu kwa makampuni ya kigeni lakini sivyo kwa makampuni ya ndani ya madini. Kubwa kabisa juu ya sera hii ni kufungua milango iliyongeza uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni Tanzania na kuiweka nchi katika orodha ya nchi zinazotambuliwa na mashirika ya bima ya kimataifa. Utawala wa fedha pia unapendelea zaidi wawekezaji wa kigeni, bila kutoa haki na usawa waa faida ya rasilimali ya madini kati ya wawekezaji wa kigeni, jamii na Serikali za mitaa. Muhimu zaidi, katika Tanzania, wawekezaji wa ndani katika sekta huujisikia wamesahaulika kwa sera hii ya sasa, na wanadai kutopatiwa motisha kama ilivyo kwa wawekezaji wa kigeni. Hivyo, mfumo wa motisha uliopo unalenga kuvutia kwa makusudi uwekekezaji kutoka nje ya nchi. Hivyo, Utafiti huu umeazimia mapendekezo manne. Kwanza, ni kwa serikali na wadau wengine kupitia upya sera na sheria ya madini na kuhakikisha haki na usawa katika kufaidi madini na rasilimali za taifa. Pili, juhudi za makusudi zinatakiwa ili kuongeza thamani ya mazao ya madini, tatu, ongezeko la makusudi katika kuunganisha sekta ya madini na sekta nyingine za uchumi wa ndani na nne, inapendekezwa kufanyika tathmini ya kimkakati ya jumla ya athari za kijamii na kimazingira katika bonde la dhahabu la ziwa Victoria ili kubaini ya mjumuiko wa athari (cummulative effects) za uchimbaji wa madini. Katika hitimisho utafiti huu unashauri kuwa utafiti wa baadaye uelekezwe juu ya mahusiano ya faida, kodi ya mapato ya kampuni na uwajibikaji wa kijamii wa makampuni ya madini ya kigeni ili kuweza kubainisha nafasi yake katika kupunguza umaskini nchini Tanzania na nchi nyingine za Afrika.